

## **AFYA YA KINYWA NA MENO WAKATI WA UJAUZITO**

Wanawake kipindi cha ujauzito wanakuwa kwenye mazingira hatarishi ya kuugua Magonjwa ya Kinywa na Meno. Magonjwa ya Kinywa na Meno kipindi cha ujauzito huleta madhara kwa mama mjamzito na mtoto aliyepo tumboni. Kwa bahati mbaya, akina mama kipindi cha ujauzito hawapati nafasi ya kuonana na Daktari wa Kinywa na Meno kwa ajili ya uchunguzi na kupata elimu sahihi ya utunzaji Kinywa chake.

Shirika la Afya Ulimwenguni linasisitiza kuwa watoa huduma ya Afya kwenye Kliniki za Afya ya mama na mtoto (Waugazi na Wakunga) wanalojukumu kubwa la kuhamasisha na kuelimisha kuhusu Afya ya Kinywa na Meno. Nchini Tanzania, waugazi na wakunga ni watu ambao hukutana na kina mama wajawazito mara nyingi katika kipindi chote cha ujauzito.

Kitita hiki kimetengenezwa kwa lugha nyepesi itakayo wawezesha Waugazi na Wakunga kutoa ushauri nasaha kuhusu Afya ya Kinywa na Meno kipindi cha Ujauzito.

### **IMEIDHINISHWA NA**



WIZARA YA  
AFYA



HOSPITALI YA  
KILUTHERI YA  
ILEMBULA



Finnish institute for  
health and welfare

